

# Je, ninapaswa kupimwa lini? Mwanafamilia Mgonjwa

## MANUKUU

[Muziki wa kusisimua]

[Masimulizi]

Je, unapaswa kupimwa COVID-19 lini?

Mtu fulani katika familia yako ameugua COVID-19. Amekuwa akikaa nyumbani (kujitenga), lakini umekuwa ukiwakaribia nyumbani.

Kwa mujibu ya masharti ya vipimo, wanafamilia wote wanapaswa kupimwa baada ya kuwa karibu na mtu nyumbani ambaye ana COVID-19.

Mtu mgonjwa anahitaji kukaa nyumbani na mbali na wengine angalau kwa siku tano (kujitenga), kwa sababu anaweza kuwaambukiza wengine wakati huu. Anapaswa pia kuvala barakoa anapowakaribia wengine nyumbani. Anaweza kuhitaji kukaa nyumbani kwa muda mrefu ikiwa bado ana dalili, au ikiwa hawesi kuvala barakoa.

Tembelea ukurasa wetu wa wavuti wa Ikiwa Wewe ni Mgonjwa

(<https://www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/sick.html>) upate maelezo mahususi kuhusu muda unaopaswa kukaa nyumbani ikiwa una COVID-19.

Ikiwa unaishi na mtu aliye na COVID-19, huenda utahitaji kuwekwa karantini baada ya mgonjwa kumaliza kutengwa kwake. Tembelea ukurasa wa wavuti wa MDH wa Karantini na Watu uliokaribiana nao upate maelezo zaidi kuhusu kuvala barakoa ukiwa karibu na wengine na urefu wa muda wa kukaa nyumbani:  
(<https://www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/close.html>)

Wanafamilia wote wanapaswa kupimwa siku tano baada ya mgonjwa kumaliza kutengwa ili kuhakikisha kuwa hakuna mtu aliyeambukizwa. Katika hali hii, siku ya mwisho ya kutengwa kwa mwanafamilia wako ni Alhamisi. Wanafamilia wote wanapaswa kupimwa siku tano baadaye, Jumanne inayofuata.

Ili upate maelezo zaidi kuhusu nyakati nyingine unazopaswa kupimwa, na mahali pa kupimiwa, tembelea ukurasa wa tovuti ya MDH ya Kupimwa COVID-19. (<https://www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/testsites/index.html>)

[Muziki wa kusisimua]

Minnesota Department of Health  
Communications Office  
PO Box 64975  
St. Paul, MN 55164-0975  
651-201-4989  
[health.communications@state.mn.us](mailto:health.communications@state.mn.us)  
[www.health.state.mn.us](http://www.health.state.mn.us)

2/2/22 (Swahili)

*Ili upate maelezo haya kwa muundo tofauti, piga simu: 651-201-4989*